Repoti ya mkutano kati ya
Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)
na
Idara ya Usalama Barabarani, Wizara ya Miundombinu
14 Januari 2008

Utangulizi

UWABA tuliandika barua kwa Waziri wa Miundombinu (Mhe Andrew Chenge) tarehe 18 Februari 2007 kuomba kukutana naye. UWABA tulipata jibu tarehe 27 Februari 2007 kuunga mkono yetu ya kuunda asasi hii muhimu hasa kama tulivyoeleza kwa nia ya kutunzaji ya mazingira, kupunguza msongomano wa magari mjini na pia kwa chombo muhimu kwa mazoezi. Waziri alisema atapenda kutana na UWABA lakini anapendekeza tukutane na idara chini ya Wizara mfano TANROADS kwanza kabla kutana naye.

Mwaka 2007 UWABA tulikutana na TANROADS, taasisi ya Dar es Salaam na makao makuu, ma tuliandika barua na tulipokea majibu mawili na maelezo mazuri kuhusu barabara za Dar es Salaam zinazojengwa.

Mwanzo wa 2008, UWABA tuliamua kuomba mkutano na idara ya usalama barabarani ya Wizara ya Miundombinu. Katibu wa UWABA alileta barua kuomba mkutano na idara hiyo kwa mkono. Ndani ya barua UWABA tulisema malengo ya mkutano ni kama yafuatayo:

- Kuwasilisha mada ya powerpoint kuhusu masuala ya wapanda baisikeli
- Kutafuta taarifa kuhusu sera na regulations za barabara ambazo zinahusu wapanda baisikeli
- Kutafuta taarifa kuhusu sera za design za barabara zinazojengwa na vipi designs hizi zinalinda usalama wa wapanda baisikeli
- Kuangalia vipi UWABA tunaweza kuendelea kutoa maoni yetu katika sera za usalama barabarani hapa Dar es Salaam

Mkurugenzi wa idara ya usalama barabarani alipokea barua hii na alitupa UWABA miadi ya jumatatu tarehe 14 Januari 2008 saa nne asubuhi. Ilikubalika kwamba mkutano utakuwa wa saa moja, including mada na mazumgumzo. Tuliambiwa wawawakilishi watano wa UWABA wanaweza kuja.

Kabla ya hapo, UWABA tulikuwa tumeandaa mada kuhusu masuala ya usalama barabarani kwa wapanda baisikeli wa Dar es Salaam. Wanachama walifanya savei za hali za barabara na tuliweka maoni yote pamoja.

Jumamosi tarehe 12 Januari kwenye mkutano wa kila wiki wa UWABA, wanachama walitoa maoni zaidi na tulirekebisha mada yetu hasa kwa ajili ya mkutano huu, na tulichagua wanachama wa kuwakilisha UWABA kwenye mkutano.

Repoti ya mkutano

Wawakilishi wa UWABA tulifika ofisi ya idara ya usalama barabarani, Wizara ya Miundombinu saa nne asubuhi kama ilivyokubalika. Wawakilishi wote wanne walijitolea na walitumia muda wao wa kazi kuja kwenye mkutano – hawalipwi kuwawakilisha wapanda baisikeli wenzao, wanajitolea. Tuliambiwa tusubiri na hatukuingia kwenye chumba cha mkutano mpaka saa tano kasoro robo. Wawakilishi watatu wa idara ya usalama barabarani walikuwepo. UWABA tulisambaza nakala za mada yetu.

Mkurugenzi wa idara ya usalama barabarani alituambia tutakuwa na dakika 15 tu, siyo saa moja kama tulikuwa tumekubaliana. UWABA tulianza kwa kujaribu kutambulisha wawakilishi wanne wa UWABA na kuomba wawakilishi watatu wa idara ya usalama barabarani kujitambulisha, lakini tuliambiwa hatuwezi kufanya utambulisho kwa sababu ya muda, basi hatujui majina ya watu wawili tulikutana nao.

Kwa sababu ya muda finyu tuliopewa ghafla, mwenyekiti wa UWABA alianza kupitia mada kwa haraka sana, na alichukua sekunde chache tu kwa kila slide, maana yake hatukuweza kujieleza vizuri. Hata wakati alijaribu kuenda haraka, alikuwa anakatishwa kila mara kwa ghafla kwa mkurugenzi wa usalama barabarani na aliambiwa kuruka vipngele vya mada.

Wakati tulipozungumzia mambo ya ushauri/uchangiahi wa washika dau, tuliambiwa kwamba UWABA hatutakuwa na nafasi ya kuchangia mawazo kwa sababu sisi si “watalaam” na hatujasoma. Tulijibu kwamba hata kama sisi si watalaaam wa sheria wala uhandisi, tuna uzoefu mkubwa wa kuendesha baisikeli kwenye barabara za Dar es Salaam na huu ni aina nyingine ya utalaam. Lakini walisema tu tena kwamba sisi si wahandisi wala wana sheria basi hakuna uwezekano kuchangia mawazo kama washika dau. Tulisema kwamaba MKUKUTA ina sera ya kusanya maoni ya washika dau na tuliambiwa kwamba idara hii “hatujaanza MKUKUTA”.

Slide moja tuliuliza nakala za regulations za barabara. Tuliambiwa kwamba “hatujafanya homework” na kwamba regulations hizi zinapatikana kutoka printer ya Serekali au duka la vitabu la Serekali au polisi wa trafiki. Tulijibu kwamba mara nyingi regulations zipo “out of print” au hazipatikani kwenye Printer ya Serekali wala Duka la Vitabu la Serekali, na kwamba tumeshaomba nakala za regulations kutoka polisi wa trafiki lakini bado hatujapewa nakala. Tuliomba msaada kutoka idara ya usalama barabarani ya Wizara ya Miundombinu kutafuta nakala za regulations lakini tuliambiwa tunapoteza muda wa serekali tu.

Tuliambiwa ghafla kuondoka kabla hatujamaliza mada.

Kwa ujumla tulikuwepo chumba cha mkutano kama dakika 15 tu na muda mwingi haukutumika kwenye mada bali kuambiwa hatujasoma wala hatujafanya “homework” na tunapoteza muda wa idara.

Mazumgumzo wa wawakilishi wa UWABA baada ya mkutano

Baada ya mkutano wawakilishi wanne wa UWABA tuliongeana kuhusu thamani ya mkutano. Wawakilishi tuliona kwamba hatujaheshimiwa kama inafaa kwa wananchi watatu wa Tanzania na wawakilishi wa kupigwa kura wa NGO wa wanachama wengi wa kuwawakilisha mahitaji ya wapanda baisikeli. Tulifikiri tutapewa nafasi ya kumaliza mada bila kubugudiwa na kuwa na mazumgumzo ya maelewano na kuheshimiana kuhusu vipi tunaweza kushirikiana kati ya UWABA na idara ya usalama barabarani kuongeza usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Baadala ya hiyo, tuliona tumepoteza muda wetu kuandaa na kuhudhuria mkutano huu. Tuliona siyo heshima kwa idara kufikiri kwamba hatuna mawazo ya thamani kwa sababu sisi hatujasoma uhandisi wala sheria, na tuliona jinsi idara walivyoongea tulijisikia kama hatujui chotochote na sisi ni wajinga. Tulishindwa kuelewa kwa nini tulipewa miadi kama idara walipanga kuendesha mkutano hivi. Tuliona kama idara ya usalama barabarani ya Wizara ya Miundombinu haitaki kusikia maoni ya wananchi au wanaotumia barabara, na haitaki kusikia maoni ya washika dau.